# K U M P I N G A

*Basi mtini Mungu. Mpingeni shetani, naye atawakimbia (Yakobo 4:7)*

Kumbuka neno la Mungu litamshinda shetani mahali popote, wakati wowote, useme tu, “ imeandikwa” Hiyo inamaliza hilo. Shetani itabidi aliumbie.” Mpingeni shetani naye atawakimbia”.

Huwezi kupata uzima ila kupitia tu kwa kristo. Na sasa Neno lake linafanya nini? Linajenga mwili wetu wa kiroho unakuwa na nguvu kadiri tunavyoshirikiana naye kumpinga shetani.

Unasema Ndugu Braham, Ni kitu gani hicho unachosema, “kuwa na ushirika katika Neno lake?” Ndiyo yeye ni Neno .
“hapo mwanzo kulikuwako na neno naye neno alikuwako kwa Mungu naye neno naye neno alifanyika mwili akakaa kwetu” Yohana 1:1-3 na tunapaswa kuula mwili wake. Na mwili wake ni Neno lake kwa sababu yeye ni Neno naye alisema katika Yohana 15:7” kama mlikaa ndani yangu na ushirika wangu, Neno langu lilikaa ndani yenu hapo sasa mnaweza kuomba mtakacho na mtatendewa hilo”. Unaona hilo hiyo ni kweli unaomba utakalo.

Unafanya nini? Unaujenga mwili wako kujikinga kutokana na … Mtu Fulani amekuja na kusema, Oh kanisa letu haliamini juu ya kupinga makelele”. Unaona umejengeka. Ni nini? Unao ushirika ndani yako lile Neno na umewekewa kinga hutokana nalo kama kundi la upuuzi linakuja ni kitu gani? Halina Neno ndani yake, hivyo una uhakika ni makosa Haijalishi inaonekana ni halisi namna gani kama sio Neno, liache peke yake (Hiyo ni sahihi) liachilie peke yake. Sijalishi limefanya nini lazima ilingane na Neno.

Adui alie kama mafuriko, kama anavyokuja leo, Mungu amesema atafaya nini? Roho wa Mungu atainua kiwango cha kumpinga. Je wewe ni mmoja wao? Ndiyo Bwana

Tunafundishwa katika kitabu cha Yakobo 4:7 kumpinga shetanui na sio atatembea na kuondoka bali atakimbia. Mpinge shetani . unampingaje shetani? Kama vilevile kapteni mkuu alivyotuagiza chukua Neno la Mungu hivyo ndivyo unavyompinga shetani kwa Neno la Mungu kapteni mkuu ametuambia namna ya kulifanya hiyo ni sahihi.

Sasa nataka kusema hili shetani yule wa kale sasa unafikiri ataenda kwa ushupavu unafikiri atashambulia mtoto? Atashambulia chochote alimshambulia Yesu Kristo .alikuja kwake na mashambulizi makali matatu (Matayo 4:1-11) ulijua hilo? Shetani hatashambulia mara moja tu atakushambulia na ugonjwa na hapa atorudi tena na kukushambulia na kusema “siku za miujiza zimepita huwezi uliopata uponyaji hakuna kitu katika hilo”. Unajua hiyo ni kweli?

Alimshambulia Yesu mara tatu. Wa kutokuamini kwake Neno la Mungu alimshambulia Yesu kwa mashambulizi makuu matatu hakika hakuliamini hilo.” Kama wewe ni” amekuja hapa mashambulizi ya nguvu kama ile wakati mwingine adui afanyavyo anakuja hapa na kusema,” ilikuwa wewe Mwana wa Mungu Nionyeshe mimi miujiza hebu niuone ukifanyika.” Ndugu alimrukia na mashambulizi makuu matatu, “ kama wewe ni”

Yesu alikuwa na imani yake kamilifu, Alikuwa waajabu sana na shetani hakukaa naye muda mrefu sana. Pale alipokuja na jambo hili kuu la ufahamu wa kiakili alikuja na udanganyifu wake kinyume na Yesu alipomuendea alijua amegusa waya wa maelfu ya volti ulimuunguza na kumrudisha nyuma tena Ndiyo **B**wana na akasema” Imeandikwa mtu hataishi kwa mkate tu” oh alipata mshituko hapo.

Mara ya pili alikuja akiwa laini kidogo aliposema ‘ sasa wewe ni mtu mkuu unaweza ukajiinua juu hapa na kuwa mtu wa maana”

Akasema “rudi nyuma yangu shetani”. Oh jamani kile alichokutana nacho na “Usimjaribu Bwana Mungu wako” unaona alimthibitishia shetani kwamba alikuwa Bwana Mungu” kwa maana imeandikwa usimjaribu…”

Sasa, kama shetani hakujua kwamba yeye ni Bwana Mungu, angesema,” Ngoja kidogo wewe siye mtu” lakini alijua vizuri zaidi kukaa na Yesu.

Alijua mahali pa kusimamia Alisema usimjaaribu Bwana Mungu wako” Na hivyo ndivyo Alivyokuwa na shetani alijua vema zaidi kusema hivyo kwa sababu kazi za Yesu zilizibitishwa kwamba yeye alikuwa Bwana Mungu.

Sasa angalia Imani kamilifu inatawala mazingira yote sasa hebu angalia unapoamini chochote unapofanya chochote na una imani na kile unachokifanya; bila kujali mazingira yakoje hilo halina uhusiano wowote na hilo unaona inatawala mazingira kama ni katika chumba cha magonjwa na Bwana amefunua kwamba hili jambo Fulani litaenda kutokea wewe linene hilo na uendelee.

“oh, linafanya…” usijiulize swali lolote. Hilo limehusisha endelea tu mbali unaona? Iinatawala mazingira yote “vema kama unafanya hili huyu na huyu wataenda kufanya…”Hilo… unaona, hilo limeshakuwa chini ya mamlaka unaona?

Imani inaamini kwamba Mungu atalitenda. Sijui atalitenda vipi lakini atalitenda kwa vyovyote.” Unaona? Inatawala mazingira yote.

Na Imani na upendo vimeshirikiana kwa sababu huwezi ukawa na Imani pasipokuwa na Upendo kwa sababu imani yako iko katika Mungu ambaye ndiye chimbuko hasa la upendo imani na upendo hutenda kazi pamoja.

Na mtu anapoishi kwa imani na atende kwa imani kiumbe kipya ndani ya kristo pale sasa unaingia kupata kitu halisi Bibi Arusi unaona unaona? Unaingia katika hali ya kunyakuliwa sasa hiyo inamaanisha kwa kila mmoja wetu siyo tu mchungaji shemasi mhariri hiyo inamaanisha kwa washirika kila mmoja anatembea duniani akiwa na Mungu peke yake. Unabatizwa katika ufalme na hakuna mtu yoyote pale ila wewe na Mungu unaona? Anatoa maagizo nawe unayachukua chochote anachosema hakuna kivuli cha shaka popote. Unatembea mbele kama Mungu anasema hivi hakuna mtu duniani awezaye kukutoa katika hilo unaendelea mbele tu.

Sasa unakuja kwenye imani kamilifu ukamilifu wa ukamili ambao hauwezi kushindwa ile mani kamwe haishindwi.

Ndiyo alikuwa wa ajabu kwao na imani yake kamilifu na ndivyo ilivyo leo kwa wale wenye imani kamilifu niwa ajabu sana kwa watu wengine.

Tunafundishwa kumpinga shetani naye atakimbia kutoka kwetu sasa " Kumpinga ni "kumkatalia" yamaanisha nenda zako mbali naye Mungu amesema jambo Fulani haijalisha anajaribu kukuambia nini hupaswi hata kumsikiliza sikio lako ni kiziwi kwa kitu kingine chochote isipokuwa kile Roho anachosema unaona? "kwake yeye aliye na sikio (anayesikiliza) asikiwe kileRoho anachoyaambia makanisa" kwa mmoja yule aliye na nguzo ya kusikilizia ambaye amepata kile Roho anachoyaambia makanisa unaona?

Mungu alimuahidi Ibrahim katika Mwanzo 22:17,…. Na uzao wako utamiliki mlango wa adui zao.

Siku moja akaja ule uzao wa kifalme wa Ibrahimu Yesu Kristo mwana wa Mungu uzao wa imani za Ibrahimu siyo kupitia Isaka mzao wa asili walifanya sehemu yao lakini hapa anakuja mmoja ambaye hakuzaliwa kwa njia ya kawaida hapo anakuja mmoja ambaye hakuzaliwa kwa tamaa ya kimwili hapo anakuja mmoja uzao wa bikira, Mwana wa Mungu mzao wa Ibrahimu jinsi alivyokuwa mtu mkuu wengineo wote wa kiasili wamezaliwa kiasili huyu mtu amezaliwa kupitia bikira alifanya nini alipokuja duniani? Alimshinda kila adui aliyekuwa ameshikwa na shetani Alishinda kila kitu.

Alifanya nini? Alikaa na kushinda magonjwa hakungekuwa na ugonjwa karibu naye popote palikuwa na ugonjwa yeye aliushinda. Alifanya nini baada ya kushinda? Alitupa sisi funguo (Amen) alisema, "chochote utakachofunga duniani nitakifunga mbinguni" Amina. Huo ni uzao wa Ibrahim alioahidiwa Roho mtakatifu akiwa ndani yetu sasa akiwa na funguo za kufungulia/ kuzuia magonjwa alishinda magonjwa, magonjwa hayawezi kusimama moyoni pake, na alisema kwamba ametupa funguo za jambo hilo kushinda magonjwa chochote utakachofunga duniani nami nitakifunga mbinguni".

Hata majaribu alijaribiwa katika kila namna kama sisi Alifanya nini? Aliyashinda alisemaje kwetu? Mpingeni shetani naye atawakimbia. Alishinda magonjwa kwa ajili yetu Alishinda majaribu kwa ajili yetu, alivunja lile lango chini na kuchukua funguo mbali na majaribu na kumpa mwaminio wa uzao wa Ibrahimu na kusema, "kama alikujaribu wewe, mpinge yeye naye atawakimbia" oh jamani. Mpinge yeye.

Alishinda vyote kifo na kuzimu. Alifufuka katika siku ya tatu akisema,"Nimeshinda na kwa sababu ninaishi mtaishi pia".

Oh ni ahadi ya namna gani hiyo ni kwa uzao wa Ibrahimu alishinda kaburi akafufuka siku ya tatu kwa kuhesabiwa haki kwetu alipofufuka alikuwa kuhesabiwa haki kwetu inatufanya tuwe watu wa namna gani? Alishinda magonjwa alishinda kifo, Alishinda kuzimu; alishinda kaburi, alishinda majaribu.

Oh sasa tu zaidi ya washindi kupitia yeye aliyetupenda sisi na aliyatoa maisha yake kwa ajili yetu (rumi 8:37) ukiwa ni uzao wa kifalme wa Ibrahimu akiwa na Roho yule wa Mungu aliye ndani yetu ambaye alikuwa ndani yake. Tu zaidi ya washindi kila lango limeshindwa kwa ajili yetu. Jambo moja pekee litupasalo kutenda ni kuimiliki, Limekwisha kushindwa, ugonjwa umeshindwa, kifo kimeshindwa, kuzimu kumeshindwa, kaburi limeshindwa;

Kila kitu kimeshindwa na tunashikilia funguo kwa neema yake je unaogopa kuziweka katika kufuli na kusema "Ninakuja katika Jina la Yesu kristo? Muombe Baba chochote kwa Jina langu Nampenda yeye".

"Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa yeye mtiwa muhuri hata siku ya ukombozi". Siyo mpaka uamsho mwingine, mpaka siku ya ukombozi (Waefeso 4:30) kwa kuwa tumebatizwa katika huyo kutokana na 1Korintho 12:13. Na ndani yake kuna utimilifu na hakuna dhambi inayotambulika ndani yake kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi kwa sababu uzao wake wakaa ndai yake; wala hawezi kutenda dhambi". (1yohana3:8) atawezaje wakati ile Ishara iko pale? Ishara ni alama ya kuwa amekubalika vema unasema,"ninatenda dhambi" vema hapo sasa hujawa na ile Ishara unaona?

Ile Ishara ni kizuizi kuonyesha kwamba ile gharama imelipwa kama shetani alijaribu kukupa hilo….fikiria hili kama shetani alijaribu kukua ugonjwa au kukupa kitu chochote unajua nini cha kufanya? Muonyeshe ishara yako na umthibitishie kwamba wewe ni zao lililonunuliwa na Mungu mpingeni shetani naye atawakimbia
(Yakobo 4:7) shikilia ishara juu ya Imani yako isiyotikiswa katika ahadi zake.

Mungu mara moja alitoa alama ya upinde wa mvua kama ishara yeye amekubalia mkweli katika ishara hiyo amefanya hivyo? Bado anafanya hivyo maelfu ya miaka hii yote Haijashindwa kamwe hata mara moja kushindwa kuonyesha hiyo alikuwa

mkweli katika hiyo Ishara, akituonyesha kwamba siku zote na kamwe hatashindwa kuheshimu ishara zake sijalishi kama Yesu hatakuja Miaka elfu kumi ijayo, unayo ishara inampasa aiheshimu hiyo ishara Haijalishi mambo mangapi yanabadilika na vipi vya zaidi anapaswa aiheshimu hiyo ishara alisema angefanya hivyo vema anategemea sisi sasa tuionyeshe ishara juu ya imani yetu tuliyopewa na Mungu kwa kila makundi yasiyoamini katika taifa na katika dunia kwao waaminio kwamba ishara na maajabu havifuatani na waaminio na kuwa wakweli kwenye hii ishara na inaonyesha hilo kwamba na gharama imekwisha kulipwa na tumekubaliwa kwa ajili ya kufufuka tukiwa na maisha ya Ishara ndani yetu.

**Nukuu za kiingereza**
"Ushiri=ka" (kitabu cha 10 na 1 seffersonville) Aya 108-111
Vita kuu sasa iliyowahi kupiganiwa uk. 54/" Imani kamilifu" Aya 114-125
"Mzee Ibrahimu" (kitabu 22 na 7) aya 61-65/ "ile ishara" (kitabu cha 19 na 12 Dallas) Aya 147-151

---

Jiwe la kiroho la kujengea na. 110 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, Yamekusanywa na Gerd Rodewald friedenstr. 69, D-75328 schomberge, Germany, Simu (+49) 72357613 Fax +(49) 72353306

---

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia
(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundihso uk. 724)

Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili andika kwa;

*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*